# Bwana alitutendea

**Katikati:Jumapili 02 ya Majilio Mwaka A,B,C (Zab.126(k)3**

**Ronjino Mhadisa**
**Don Bosco Choir**
**Cathedral Arusha**
**19/10/2024**







**1.Bwana alipowarejeza mateka wa Sayuni,**
**Tulikuwa kama waotao ndoto.**
**Ndipo kinywa chetu kilipojaa kicheko,**
**Na ulimi wetu kelele za furaha.**

**2.Ndipo Mataifa waliposema,**
**Bwana amewatendea mambo makuu.**
**Bwana alitutendea mambo makuu,**
**Tulikuwa tukifurahi.**

**3.Ee Bwana uwarejeze watu wetu,**
**Waliofungwa kama vijito vya kusini.**
**Wapandao kwa machozi,**
**Watavuna kwa kelele za furaha.**

**4.Ingawa mtu anakwenda zake akilia,**
**Azichukuapo mbegu za kupanda.**
**Hakika atarudi kwa kelele za furaha,**
**Aichukuapo miganda yake.**